TANGAZO LA SERIKALI NA. 279 la tarehe 7/4/2023

SHERIA YA MAMLAKA NA MAJUKUMU YA MSAJILI WA HAZINA,

(SURA YA 370)

# HATI YA UHAMISHO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(2))*

HATI YA UHAMISHO WA VIWANJA VILIVYOSAJILIWA KWA MAJINA YA SHIRIKA LA RELI TANZANIA KWENDA WAKALA WA MAJENGO TANZANIA YA MWAKA 2023

Sura ya 370 na Sura ya 257

**AMBAPO,** kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina ikisomwa pamoja na Sheria ya Mashirika ya Umma, mali zote za Serikali zimewekwa chini ya umiliki wa Msajili wa Hazina;

Sura ya 370

**AMBAPO,** Rais anaweza, kwa mamlaka aliyopewa chini ya kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina, kumpa Msajili wa Hazina maelekezo ya kuondosha mali za uwekezaji au mali yoyote inayomilikiwa na Msajili wa Hazina chini ya udhamini, na Msajili wa Hazina atatekeleza maelekezo hayo;

**NA AMBAPO,** Serikali imeona kuwa inafaa kwamba Viwanja Na. 153 na 154 chini ya Hati Miliki Na. 50401 vilivyopo mtaa wa Diwani na Ubene eneo la Chang'ombe vilivyo chini ya umiliki wa Shirika la Reli Tanzania kuhamishiwa kwa Wakala wa Majengo Tanzania kwa lengo la kumilikishwa kwa Vera Lymo Shadrack na Stephano Paul Mboma;

**HIVYO BASI,** imeelekezwa kama ifuatavyo:

*Tangazo la Serikali Na. 279 (linaendelea)*

Jina

1. Hati hii itajulikana kama Hati ya Uhamisho wa Viwanja Vilivyosajiliwa kwa Majina ya Shirika la Reli Tanzania Kwenda Wakala wa Majengo Tanzania ya Mwaka 2023.

Uhamisho wa viwanja

2. Viwanja vilivyoainishwa katika Jedwali la Hati hii ambavyo kwa sasa vinamilikiwa na Shirika la Reli Tanzania, bila uthibitisho wa ziada na kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Hati hii, vinahamishiwa kwa Wakala wa Majengo Tanzania kwa lengo la kumilikishwa kwa Vera Lymo Shedrack na Stephano Paul Mboma.

**JEDWALI**

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

| Mkoa | Na. | Hati Miliki na Maelezo ya Kiwanja | Taasisi Inayohamishiwa |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | 1. | Viwanja Na. 153 na 154 chini ya Hati Miliki Na. 50401 vilivyo mtaa wa Diwani na Ubena eneo la Chang'ombe, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke, Dar es Salaam | Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) |

**KWA AMRI YA RAIS**

Dodoma,
28 February, 2023

MOSES M. KUSILUKA
*Katibu Mkuu Kiongozi*